Kamusi

Fafanuzi ya

Misemo na Nahau

F. M. Kagwa

Gichohi Waihiga

Target
PUBLICATIONS LIMITED
Unveiling your Potential

Kimechapishwa na:

Target Publications Limited,
Jengo la Kipro, Barabara ya Sports,
Westlands
S.L.P. 13433-00800
Nairobi, Kenya
Simu: +254-20-4441345
Kipepesi: +254-020-4441622
Baruapepe: info@targetpublications.co.ke
Tovuti: www.targetpublications.co.ke

© F. M. Kagwa, Gichohi Waihiga, 2011

Haki zote zimehifadhiwa. Ni marufuku kuiga, kunakili, kudurufu, kufotoa, kupigisha chapa, kutafsiri au kukitoa kitabu hiki kwa mbinu zozote zile bila idhini kwa maandishi kutoka kwa mchapishaji.

Haki za kimaadili za waandishi zimetambuliwa.

Chapa ya kwanza 2011

ISBN: 978 9966 002 42 6

Kurasa zimeruwazwa na kusanifiwa na Peter Mwendwa
Jalada limesanifiwa na Mbugua Njache

Kimepigwa chapa na:

Printwell Industries Limited
Eneo la Viwandani
S.L.P. 5216-00506
Nairobi, Kenya.

PL8703
.K337
2011

Utangulizi

Misemo na nahau ni vitanzu vya semi za Kiswahili. Semi ni mojawapo ya tanzu za fasihi simulizi. Maana yake ni kuwa, misemo na nahau hupokezanwa kutoka kizazi hadi kingine, kwa njia ya mdomo. Hii haimaanishi kuwa misemo na nahau zinazopatikana katika Kiswahili ni zile za jadi tu na kuwa hazikui na kuongezeka. Binadamu ana uwezo wa kukuza semi zake na kuendelea kuzipitisha kutoka kizazi hadi kingine.

Kufikia sasa, njia za kupitisha semi za Kiswahili, kama zilivyo semi katika lugha zingine, zimeongezeka. Pamoja na kuwa njia ya kupitishwa kwa mdomo kutoka kizazi hadi kingine inaendelea kutumiwa, siku hizi njia hii inachukua nafasi ndogo ikilinganishwa na njia kama vile kuandika vitabuni, majaridani na kunakili katika vyombo vya kielektroniki. Muhimu hata hivyo ni kuwa misemo na nahau zimekuwapo na zitaendelea kuwapo katika jamii zetu.

Maana ya misemo na nahau

Msemo ni neno au kifungu cha maneno kinachotumiwa na jamii mahususi kwa maana na namna maalum. Misemo na nahau huwa na maana fiche ambayo humbidi anayezisikia kuwa mweledi wa lugha inayozitumia au kufikiria kwa makini ili kuelewa. Sifa ya kuwa na maana fiche inafanya msemo na nahau kuwa aina fulani ya fumbo, hivyo ni mojawapo ya tamathali za semi.

Licha ya kuwa na maana fiche, msemo hutumia mpangilio wa kawaida wa sentensi ya Kiswahili na upatanisho wa kisarufi. Maana yake ni kuwa msemo unaweza kueleweka kwa urahisi. Kwa mfano, msemo siri na moyo wako ni maneno yanayoeleweka moja kwa moja, kuwa mtu aiweke siri yake moyoni, asiitoe. Msemo zua vita una maana ya "anzisha au sababisha vita".

Wakati mwingi, neno "msemo" huchukuliwa kwa maana pana inayojumuisha semi ziitwazo nahau. Kwa wengi, msemo unaweza kuitwa nahau, nayo nahau kuitwa msemo. Ingawa ni vigumu kuweka mpaka bayana baina ya semi hizi mbili, kuna semi ambazo kwa hakika ni nahau na wala si misemo. Hili linaweza kuthibitishwa na maana ya neno "nahau" ambayo ni "neno au kifungu cha maneno ambayo yana maana maalum isiyolingana moja kwa moja na maana za kawaida za maneno hayo". Hii inamaanisha kuwa maana ya nahau haijitokezi waziwazi. Kwa mfano, maneno piga chafya hayamaanishi "chapa hewa itokayo mdomoni au puani kwa ghafla". Maana yake ni "chemua"; wala maana ya enda kombo si "kwenda mahali fulani panapoitwa Kombo". Maana yake ni "mambo kuharibika". Kwa jumla hata hivyo, misemo na nahau hutaka makini ili kupata maana kamili.

Kama inavyodhihirika katika maelezo haya, msemo haufai kuitwa semi moja kwa moja, kwa kuwa semi ni jumla ya ujumbe unaowasilishwa kwa njia ya